

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



BUNGE LA TANZANIA

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU MAPENDEKEZO YA
MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA PAMOJA NA MWONGOZO WA
KUTAYARISHA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18.**

Ofisi ya Bunge,
S. L. P 941,
DODOMA

Novemba, 2016.

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 94(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti Kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa pamoja na Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/18.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya bajeti imeusoma na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18 iliyotayarishwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa muhtasari Mapendekezo hayo yanatoa maelekezo kwa Maafisa Masuhuli wa Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma namna bora ya kuandaa na kutekeleza mipango na bajeti itakayoendana na vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21); ambavyo ni kuwa na viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa misingi ya uchumi; kufungamanisha maendeleo ya uchumi na rasilimali watu; kujenga mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji pamoja na usimamizi wa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mapendekezo haya yanaelekeza vyombo husika utaratibu wa utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini za Mipango na Bajeti zao ili kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha za Serikali, kwa kuzingatia miongozo ya kisheria; pamoja na namna bora ya ukusanyaji wa mapato na utengaji wa rasilimali fedha kugharamia miradi ya maendeleo; kutoa mwongozo wa kutayarisha Mipango ya Maendeleo kwa Wizara, Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi na wadau wengine; pamoja na mapitio ya ukuaji wa Uchumi Jumla kwa kuzingatia utekelezaji wa sera za fedha na kodi tukielekea mwaka 2017/18.

2.0. MAPITIO YA HALI YA UCHUMI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2016

Mheshimiwa Spika, Takwimu kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu zinaonyesha kwamba, katika nusu ya kwanza ya mwaka 2016 (Januari hadi Juni) Pato Halisi la Taifa lilikuwa shilingi trilioni 23.5 ikilinganishwa na shilingi trilioni 22.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Sekta zilizokuwa na ukuaji mkubwa ni pamoja na usafirishaji na uhifadhi wa mizigo (asilimia 17.4) na uchimbaji madini na mawe (asilimia 13.7). Aidha, shughuli zilizokuwa na ukuaji mdogo ni pamoja na huduma za chakula na malazi (asilimia 0.6) pamoja na usambazaji maji safi na

uthibiti wa maji taka. Mwenendo wa mfumuko wa bei umekuwa wa kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, Kamati ingependa kutoa angalizo kuhusu kushuka kwa wastani wa pato kwa kila mtu katika Dola za Kimarekani kutoka Dola za Kimarekani 1,047 mwaka 2014 hadi Dola za Kimarekani 966.5 mwaka 2015 ambako kunaelezwa kuwa kulitokana na kushuka kwa thamani ya shilingi. Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani iliendelea kupungua katika kipindi chote cha mwaka 2015 na nusu ya kwanza ya mwaka 2016. Dola moja ya Marekani ilinunuliwa kwa wastani wa shilingi za Tanzania 2,179.0 Julai 2016 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,086.4 Julai 2015.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada nzuri zinazochukuliwa na Serikali katika kuongeza Pato la Taifa na kupunguza Mfumuko wa bei; Kamati inaona bado kuna changamoto kubwa katika eneo hili hasa katika upatikanaji wa vyanzo vipya vya mapato. Serikali imekuwa ikitegemea Mapato yake kwa kuibua Mapato ya Ndani zaidi (*Tax Revenue*) kuliko kuangalia vyanzo vingine vya mapato (*Non Tax Revenue*) vitakavyosaidia kugharamia Bajeti ya Serikali. Ipo haja ya kuona kodi zinazobuniwa zinasaidia kuongeza ari ya uzalishaji, ujasiriamali na uwekezaji na hivyo kuongeza Pato la Taifa, Aidha, ukuaji wa uchumi ujielekeze zaidi katika kuongeza

kipato kwa Mtanzania na hivyo kufikia malengo tuliyojiwekea katika Dira ya Maendeleo kuwa ifikapo mwaka 2025 pato la kila mtanzania liwe limefikia Dola za Kimarekani 3,000.

3.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MWONGOZO WA KUTAYARISHA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2017/18

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuandaa na hatimaye kupitishwa na Bunge lako Tukufu Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015. Sheria hii pamoja na Kanuni zake vitasaidia kuhakikisha usimamizi na uwajibikaji katika hatua zote za mchakato wa bajeti unazingatiwa. Vilevile Kamati inaipongeza Serikali kwa kuandaa Mfumo wa Programu wa Kibajeti ili kuwezesha utekelezaji wa bajeti kwa kuzingatia vipaumbele na kuanzisha utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha awamu ya nne. Mifumo hii kwa ujumla itasaidia sana kuongeza ufanisi, uwajibikaji na uwazi wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Baada ya pongezi hizi, Kamati ingependa kutoa maoni/ ushauri na mapendekezo kuhusu Mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Mwaka 2017/18 kama ifuatavyo;

3.1 Makisio ya awali ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/18

Mheshimiwa Spika, makisio ya awali ya Bajeti ya Serikali yanaonyesha kuwa jumla ya shilingi **trilioni 32.946** zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18 ambapo kati ya fedha hizo shilingi **trilioni 20.872** sawa na **asilimia 63** ya bajeti yote zitatokana na mapato ya ndani. Kamati inaamini kuwa, Serikali imepanga kuongeza mapato yake ya ndani hasa yale yatokanayo na kodi kwa kupanua wigo wake wa kukusanya kodi kwa kuja na vyanzo vipya ambavyo havitakuwa kero kwa wafanyabiashara na wananchi wote kwa ujumla ili kuweza kufikia lengo la mapato yatokanayo na kodi lililoongezeka kwa **asilimia 16.532** kutoka shilingi **trilioni 15.105** mwaka 2016/17 hadi shilingi **trilioni 18.097** mwaka 2017/18. Aidha pamoja na hatua hii muhimu ni vema Serikali ikajielekeza katika kuangalia pia vyanzo vingine vya mapato (*Non Tax Revenue*) vitakavyosaidia kugharamia Bajeti ya Serikali.

3.2 Mwenendo wa Mikopo

Mheshimiwa Spika, Takwimu zinaonyesha kuwa Serikali imepanga kukopa ndani kiasi cha shilingi **trilioni 6.28** (trilioni 4.435 kulipia hati fungani na dhamana zilizoiva na shilingi **trilioni 1.859** ambayo ni sawa na **1.5%** ya Pato la Taifa kwa ajili

ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo) kwa mwaka 2017/18. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la **asilimia 14.49** ukilinganisha na kiwango cha mikopo ya ndani iliyokopwa katika mwaka wa fedha 2016/17 cha shilingi **trilioni 5.37**. Kamati haipingani na mpango wa Serikali wa kukopa kiasi cha shilingi **trilioni 2.080** (Dola za Kimarekani 900) kutoka katika vyanzo vyake vya nje ili kugharamia utekelezaji wa miradi yake ya maendeleo. Kamati ingependa kuishauri Serikali kupunguza kukopa zaidi katika vyanzo vya ndani.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa, ukopaji mkubwa wa ndani unapunguza uwezo wa wafanyabiashara, wajasiriamali na wananchi kwa ujumla kuweza kukopa katika Taasisi za Fedha hapa nchini. Taasisi za Fedha zinaona ni salama zaidi kuikopesha Serikali kuliko wananchi ili kupunguza 'risk' zinazojitokeza katika ukusanyaji na usimamizi wa mikopo hiyo. Ili kutatua changamoto hii ni vema Serikali ikatumia nafasi yake ya uwezo wa kukopa nje ya nchi ili kugharamia miradi itakayoleta matokeo ya haraka ya kiuchumi yenye *multiplier effect*. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka zoezi la *Sovereign Rating* ili kuiwezesha kukopa zaidi kutoka katika vyanzo vya nje ili iwezekugharamia miradi yake ya maendeleo na hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa kiwango cha fedha itakachokopa kutoka katika vyanzo vya ndani.

3.3 Uwasilishaji wa Mapato ya Serikali kwenda Benki Kuu (BOT)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono hatua ya Serikali ya kuanzisha utaratibu wa Wizara, Taasisi na Mashirika yote ya Umma kutakiwa kuwasilisha Benki Kuu mapato yao yote wanayoyakusanya kila baada ya masaa 24 baada ya kukusanya. Lengo la utaratibu huu ni kuiwezesha Serikali kuwa na udhibiti wa fedha za umma. Utaratibu huu pia utaiwezesha Serikali kujua inafedha kiasi gani zilizokusanywa wakati wowote. Hata hivyo Kamati inapenda kuishauri Serikali kuhakikisha inapeleka haraka iwezekanavyo fedha za matumizi ya Wizara, Taasisi na Mashirika hayo kadiri ya mipango kazi inavyoonyesha na kadiri walivyopitishiwa na Bunge katika bajeti zao ili kuepuka kukwamisha utekelezaji. Aidha Kamati inaitaka Serikali kuwasilisha Bungeni Mwongozo au Utaratibu wa kubakisha fedha (*Retention*) kwenye baadhi ya Wizara na Taasisi za Serikali zenye uhitaji wa fedha hizo kwa shughuli maalumu kwa mujibu wa Sheria husika.

3.4 Kodi ya Majengo

Mheshimiwa Spika, Serikali imeeleza kuwa itaendelea na utaratibu iliouanzisha katika mwaka wa fedha wa 2016/17 wa

ukusanyaji wa kodi ya majengo kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza utekelezaji wa jambo hili kwa TRA kuanza kukusanya katika maeneo machache. Hii itaiwezesha TRA kujipanga vizuri kabla ya kuanza kukusanya maeneo yote. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu maalum utakao oneshana namna TRA watavyoendelea kukusanya katika maeneo yaliyosalia (Manispaa, Halmashauri na Miji Midogo). Aidha, Kamati ingependa kurudia ushauri wake iliutoa mwaka jana kwa Serikali kuhusu majengo ambayo hayajafanyiwa uthamini kukusanya viwango vya kodi vinavyofanana kwa majengo ya kila kundi. Vile vile katika ufanyaji tathmini, Serikali izingatie hali ya uchumi wa eneo husika, thamani ya ardhi na thamani ya nyumba yenyewe katika eneo husika.

3.5 Serikali kuhamia Makao Makuu Dodoma

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono mpango wa Serikali kuhamishia shughuli zake Makao Makuu ya Serikali - Dodoma kutoka Dar es salaam. Aidha, Serikali imeainisha namna (utaratibu na ratiba) itakavyotekeleza jambo hili kwa awamu katika muda mfupi na wa kati na hivyo kutoa fursa kwa Wizara husika kujipanga na kuwezesha utekelezaji wa uamuzi huu. Pamoja na nia hii nzuri ya Serikali, Kamati ya Bajeti inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha za matumizi

mengineyo (O.C) kwa mafungu husika ili kuweza kugharamia mpango huu vizuri hasa kwa upande wa malipo ya stahili za watumishi watakaohamishwa. Kamati inatoa pendekezo hili kwasababu Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/18 kuwa fedha za matumizi mengineyo (O.C) zimepungua kutoka **shilingi trilioni 2.547** zilizopitishwa mwaka 2016/17 hadi **shilingi trilioni 2.214** zinazopendekezwa kwa mwaka 2017/18.

3.6 Mikakati ya Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

Mheshimiwa Spika, Mwongozo umeainisha mikakati na hatua mbalimbali za kuongeza na kuimarisha ukusanyaji wa mapato kupitia Wizara ya Fedha na Mipango. Mikakati hiyo ni pamoja na kupitia upya ada, ushuru na tozo ili kuzirekebisha ziendane na maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii, kufanya mapitio ya mikataba yote iliyopewa misamaha ya kodi ili kutathmini faida zake na kutoingia mikataba inayohusisha misamaha ya kodi bila idhini ya Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa kodi, ada, ushuru na tozo ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato. Kamati inakubaliana na maelekezo ya Serikali kwa Wizara na Taasisi zake, Hata hivyo msisitizo zaidi uwekwe katika kukamilisha mifumo ya usimamizi na malipo ya fedha kwa njia ya vifaa vya kielektroniki ili kuongeza na

kufuatilia mapato yanayokusanywa na Taasisi na mamlaka mbalimbali za Serikali. Aidha Serikali iendeleo kuhamasisha na kuongeza matumizi ya mashine za EFD na wananchi kwa ujumla kudai risiti halali pale wanaponunua bidhaa. Maeneo yenye mianya ya upotevu wa fedha kama vile uwepo wa bandari bubu na biashara za magendo kupitia mipaka yetu yadhibitiwe kikamilifu ili kuongeza upatikanaji wa mapato ya Serikali.

3.7 Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanisha namna itakavyoshirikiana na Sekta binafsi katika kuibua na kugharamia miradi kwa utaratibu wa Ushirikiano baina yake na Sekta ya Umma na Binafsi (PPP). Pamoja na kwamba kuna ongezeko la mitaji ya uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje na ile ya ubia, bado kuna ushiriki hafifu wa sekta binafsi katika kugharamia miradi ya maendeleo pamoja na miradi mingi kutokidhi vigezo vya PPP vilivyowekwa na Serikali. Kamati inaona hali hii imechangiwa na kutokuwa na mazingira wezeshi ya uwekezaji na ufanyaji biashara; uhaba wa miundombinu (barabara, maji na umeme); uwepo wa kodi zinazobadilika mara kwa mara; urasimu wa upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji; na uwezo mdogo wa kifedha na taaluma kwa sekta binafsi za ndani. Kamati ingependa kuona

kuwa mwongozo huu utasimamia kikamilifu katika kuondoa matatizo haya ukizingatia kuwa tunaelekea katika utekelezaji wa Mpango wa pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano wenye lengo la kuhakikisha tunakuwa na uchumi imara wenye uwezo wa kuhimili ushindani kupitia ukuaji wa uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Serikali imepanga kuongeza ushiriki wa Sekta binafsi katika kutekeleza Mpango wa maendeleo wa Taifa kutoka shilingi trilioni 6.8 mwaka 2016/17 hadi shilingi trilioni 7.4 mwaka 2017/18. Hata hivyo, takwimu zinaonyesha kuwa ushiriki wa Sekta binafsi bado ni mdogo. Kamati inaishauri Serikali kupunguza kiwango ambacho imekiweka kama mchango wa Sekta Binafsi katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2017/18. Kamati inaishauri Serikali iboreshe mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji ili kuiwezesha Sekta Binafsi kutoa mchango wake unaostahili katika kukuza uchumi wa nchi yetu.

3.8 Kuimarisha uchumi kupitia Sekta ya Viwanda

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba msukumo wa kipekee kwa Serikali ya awamu ya Tano ni kuhusu ujenzi wa uchumi wa viwanda na maendeleo ya rasilimali watu '*Nurturing Industrialization for Economic Transformation and Human Development*'. Kamati ingependa kuona ni kwa namna gani mwongozo huu wa maandalizi ya Mpango na Bajeti umejielekeza katika kuhakikisha unatanzua vikwazo vya ukuaji wa uchumi wa viwanda hasa katika sura zifuatazo:-

- kuandaa mpango mkakati wa kuanzisha, kukuza, kuviendeleza na kuvilinda viwanda nchini;
- kukuza na kuendeleza viwanda vyenye uzalishaji mkubwa, wa kati na mdogo; ikiwa pamoja na uanzishwaji wa viwanda vipya;
- kuboresha miundombinu ya kukuza sekta ya viwanda hasa kwa upande wa maji, barabara na umeme;
- kurekebisha Sheria, tozo na ada mbalimbali zitakazoweza uvutiaji wa uwekezaji wa viwanda vikubwa, vya kati na vidogo;
- kurekebisha Sheria za Ardhi ili kuruhusu uwekezaji mkubwa katika kilimo pamoja na kuhamasisha kilimo cha umwagiliaji ili kuwepo na uhakika wa upatikanaji wa malighafi za viwanda;
- kuhakikisha kuna uhakika wa upatikanaji wa masoko ya bidhaa zitakazozalishwa na viwanda vyetu nchini;

- Kusimamia upatikanaji wa wataalamu wa viwanda wa daraja la juu, kati na la chini ili kuongeza ufanisi wa uzalishaji viwandani katika sekta mbalimbali za viwanda;
- kuhamasisha utafiti na matumizi ya teknolojia bora itakayolinda afya ya mlaji na mazingira;

4.0. MAONI NA USHAURI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2017/18.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia na kufanya uchambuzi wa mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2017/18. Mapendekezo haya yanalenga kutoa mwongozo wa kutayarisha Mipango ya Maendeleo kwa Wizara, Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21). Kwa kuzingatia mapendekezo haya, Kamati ingependa kutoa maoni na ushauri ufuatao;

4.1. Ujumuishwaji wa Vipaumbele vya Mpango wa Mwaka unaoendelea

Mheshimiwa Spika, Kamati inaiunga mkono Serikali kwa kuchagua vipaumbele vichache vitakavyotekelezwa kwa kipindi husika. Lengo la kuchagua vipaumbele vichache ni kuwezesha rasilimali chache zilizopo zilete tija na matokeo chanya. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa,

Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Mwaka 2017/18 yanazingatia kuondoa changamoto zilizojitokeza kwenye kutekeleza vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17. Aidha, kwa sasa Serikali inaandaa bajeti kwa kuzingatia Mfumo wa Programu (Programme Based Budget –PBB) ili kutekeleza Bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopo katika kutoa huduma kwa umma. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha program hizi ambazo zimeanza kwa majaribio katika Wizara sita zinashabihiana na vipaumbele tulivyojiwekea katika mapendekezo ya mpango huu.

4.2. Viwanda vya Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda

Mheshimiwa Spika, Nchi yoyote inayotaka kupiga hatua za haraka kiuchumi ni sharti iwekeze vya kutosha katika viwanda. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua hilo na kuja na mikakati thabiti itakayoweza nchi yetu kufanya mapinduzi ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, wajasiriamali wetu wana mitaji midogo na hawana teknolojia ya hali ya juu, hivyo viwanda vidogo vidogo ni moja ya suluhisho muhimu la kuweza kuongeza ushiriki wao katika mageuzi ya viwanda katika nchi yao. Viwanda vidogo vitakavyoanzishwa na wajasiriamali wetu siyo tu vitaliingizia Taifa mapato kupitia kodi bali vitaongeza

ajira, vitatumia malighafi zinazozalishwa hapa hapa nchini pamoja na kupunguza au kuacha kabisa kuagiza nje ya nchi bidhaa ambazo ni rahisi kuzalishwa hapa nchini kwa mfano samani, vibiriti, siagi, jibini, *tomato/chili sauce*, *toothpick*, vijiko, sahani, sufuria n.k. Jambo la msingi ni kuunganisha mnyororo mzima wa uzalishaji kuanzia kwa mzalishaji wa malighafi kwenda kwa wazalishaji katika viwanda vidogo na mwisho kwa mlaji/mtumiaji.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Mpango huu yamelenga kutekeleza mradi wa Magadi Soda katika bonde la Engaruka, mradi wa kufufua kiwanda cha General tyre, uendelezaji wa viwanda vidogo vidogo- SIDO, uendelezaji wa Sekta za nguo na mavazi, ngozi na bidhaa za ngozi pamoja na mafuta ya alizeti nchini pamoja na ubainishaji wa mnyororo wa thamani wa zao angalau moja kwa kila Halmashauri. Hata hivyo, ukifuatilia kwa makini mapendekezo yaliyopita yamekuwa yakirudia rudia bila utekelezaji. Kamati inaishauri Serikali kuwa mapendekezo ya mpango huu yaonyeshe mkakati na muda wa kukamilisha miradi hii ikiwemo upatikanaji wa fedha za kumaliza miradi husika.

4.3. Kufungamanisha Maendeleo ya Uchumi na Rasilimali Watu

Mheshimiwa Spika, Hakuna maendeleo yanayoweza kupatikana katika nchi yoyote kama rasilimali watu itakuwa haijaelimishwa vya kutosha na haina afya bora. Kamati inaunga mkono Mpango wa Serikali wa kuboresha elimu na Mafunzo ya ufundi kwa kuimarisha mifumo na miundombinu katika shule za Awali, Msingi na Sekondari na vyuo. Vilevile Kamati inaunga mkono kujenga, kukarabati na kuboresha Hospitali za Rufaa na upatikanaji wa maji safi na salama na kuondosha maji taka.

Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya muda wa kati na muda mrefu ili kutatua changamoto inayoweza kujitokeza kwaongezeko la wanafunzi wanaopata nafasi za kujiunga katika Vyuo vya Elimu ya Juu. Suala la mikopo inayotolewa kwa wanafunzi wa elimu ya juu imeonekana kuwa ni changamoto kutokana na kwanza wigo kuwa mdogo, vigezo kutozingatiwana kukosekana kwa ufuatiliaji kwa waliopokea mikopo hiyo. Upo umuhimu wa Serikali kuhakikisha kuwaUpatikanaji wa mikopo unaongezeka kwa kuongeza wigo na kuzingatia vigezo vya wahitaji ili kuwezesha wanafunzi wengi kupata mikopo. Aidha, Serikali ihakikishe inaweka utaratibu wa kufuatilia wakopaji kupitia vitambulisho vya Taifa ili walio kopa warejeshe na hivyo kufanya mikopo hiyo kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, Mwaka jana wakati wa majadiliano ya mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 kulikuwa na kilio kikubwa kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusu upungufu mkubwa wa Zahanati na Vituo vya Afya hapa nchini. Serikali iliahidi Bunge kwamba italifanyia kazi suala hili kwa kufanya tathmini ya kina ili kujua mahitaji halisi pamoja na gharama ya ujenzi wake. Ni matumaini ya Kamati kuwa Serikali imekamilisha tathmini yake na itakuja na mpango mahsusni wa utekelezaji wa ujenzi wa Vituo vya Afya kila Kata na Zahanati kila kijiji na kuujumuisha kwenye Mpango wa Maendeleo unaokuja.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliamua kutenga shilingi milioni 50 kwa kila Kijiji, Mitaa na Shehia kwa upande wa Zanzibar kama Mfuko wa Uwezeshaji (*Revolving Fund*) kwa ajili ya kukopesha vikundi vya wajasiriamali kupitia ushirika wa kuweka na kukopa. Mwaka 2016/17 Serikali ilianza kutekeleza mpango huu kwa kutenga shilingi **bilioni 59** pekee ili kuipa nafasi ya kuweza kuandaa utaratibu utakaofaa wa namna ya ugawaji wa fedha hizo, pamoja na usimamizi wake. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha maandalizi ya utaratibu huo na kuanza kutenga kiasi cha shilingi **bilioni 200** kila mwaka kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 ili kuweza kukamilisha upelekaji wa fedha hizo kwenye maeneo husika katika kipindi cha miaka minne iliyosalia.

4.4. Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji wa Biashara na Uwekezaji na ushiriki wa Sekta Binafsi

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kuweka mazingira bora yatakayo iwezesha Sekta binafsi kuwekeza pamoja na kufanya biashara kwa urahisi. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha miundombinu ya usafirishaji (barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege), kuboresha upatikanaji wa umeme wa kutosha na wa uhakika, kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji, kuweka sheria za fedha na kodi zinazo tabirika (zisizo badirika mara kwa mara), kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa mali ghafi kwa ajili ya viwanda na kunakuwa na sheria bora za ajira.

Mheshimiwa Spika, Mwenendo unaonesha kuwa ushiriki wa sekta binafsi katika kutekeleza mpango wa mapinduzi ya viwanda nchini utachukua miaka mingi sana kufikia malengo yake ama isiyafikie kabisa. Duniani kote, hakuna nchi yeyote inayoweza kupiga hatua za Kiuchumi bila ya kuwa na msukumo mkubwa katika uwekezaji wa viwanda kupitia sekta binafsi hasa tukizingatia inachangia kuongeza mapato na ajira katika uchumi. Mapendekezo ya Mpango yaagize mambo yatakayo fanyika katika kuweka mazingira wezeshi yatakayo wezesha Sekta Binafsi kufanya kazi yake. Maeneo

muhimuni yenye viashiria vya kufanya biashara kama vile kufungua au kufunga biashara, upatikanaji wa Vibali vya biashara, upatikanaji mikopo, kulinda wawekezaji, ulipajikodi, mauzo ya ndani na nje ya nchi na utekelezaji wa mikataba ya biashara. Ripoti ya Benki ya dunia ya Kufanya Biashara ya mwaka 2015 (*Doing Business Report 2015*) inaonyesha Tanzania tunashika nafasi ya 139 kati ya nchi 189 duniani na inashika nafasi ya 15 kati ya nchi 47 za kusini mwa Jangwa la Sahara katika jitihada za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Tupo nyuma sana! Ili tuweze kuvutia wawekezaji wengi katika viwanda ambavyo tunatarajia kuvianzisha ni lazima tuwe na mkakati madhubuti wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

4.5. Miradi Mikubwa ya Kielelezo

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono mpango wa Serikali wa kuchagua miradi mikubwa ya kielelezo (*Flagship projects*) na kulinda bajeti zake (*ringfence*). Utekelezaji wa Miradi hii mahsusuni unalenga kufanikisha utekelezaji wa Mpango na kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Miradi hiyo niifuatayo;

4.5.1 Mchuchuma na Liganga

Mheshimiwa Spika, Miradi ya makaa ya mawe na chuma ya Liganga na Mchuchuma ni moja ya miradi mikubwa ya kielelezo iliyopangwa kutekelezwa. Mradi wamakaa ya mawe wa Mchuchuma utakapokamilika utawezesha uzalishaji wa **MW 600** ambazo zitasaidia sana kupunguza tatizo la upatikanaji wa umeme nchini. Mradi wa chuma wa Liganga utakaozalisha chuma utakuwa ni mkombozi mkubwa kwa kutoa mali ghafi ya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zitokanazo na chuma kama vile nondo. Pamoja na umuhimu mkubwa wa miradi hii mipango ya utekelezaji wake imekuwa ya kusuasua sana. Kumekuwa na tatizo la muda mrefu la kutolipa fidia kwa wananchi wanaotakiwa kuhamishwa katika maeneo miradi hiyo. Kamati inaishauri Serikali kuweka muda maalum (*timeframe*) wa ulipaji wa fidia pamoja na kukamilisha mazungumzo yake kuhusu Mkataba wa Mauziano ya umeme utakaozalishwa (PPA).

4.5.2. Maeneo Maalum ya Uwekezaji na Viwanda vidogo vidogo

Mheshimiwa Spika, Moja ya njia madhubuti ya kuiwezesha nchi kuingia haraka katika uchumi wa viwanda ni kupitia uwekezaji katika maendeleo ya Viwanda vidogo vidogo, kuboresha uwekezaji katika maeneo ya *Export Processing Zones - EPZ* pamoja na Maeneo maalum ya uwekezaji

(*Special Economic Zones – SEZ*). Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka uendelezaji wa maeneo haya likiwemo lile la Bagamoyo SEZ kwa kukamilisha ulipaji fidia wa eneo la uwekezaji na kuanza utekelezaji wa mradi wenyewe. Aidha, Serikali itenge maeneo mengine kila Mkoa na kuyapanga (*Classify*) kulingana na mazao au bidhaa zitakazozalishwa katika Mkoa husika na kuyaendeleza kwa kuyawekea miundombinu kama vile maji, umeme na barabara/reli ili kurahisisha uwekezaji katika maeneo hayo.

4.5.3 Kituo cha Biashara na Huduma Kurasini

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukamilisha ulipaji fidia kwa wananchi waliopisha mradi huu. Hata hivyo Kamati inasikitishwa na muda mrefu unaochukuliwa na Serikali katika uendelezaji wa eneo hili muhimu. Kamati inasisitiza juu ya Serikali kuona umuhimu wakuhakikisha malengo ya mradi huu yanatimizwa kwa kuzingatia kuwa mwekezaji wa awali kutoka China alikwisha ondoka. Hivyo, ni wakati sasa wa Serikali kuhuisha mazungumzo ili mwekezaji mpya apatikane kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wa mradi huu.

4.5.4. Uboreshaji wa Miundombinu ya Usafirishaji

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono mpango wa Serikali wa kuboresha miundombinu ya usafirishaji kwa

kujenga reli ya kati kwa *standard gauge*, kujenga barabara za lami na kuboresha shirika la ndege la Taifa (ATCL) kwa kuweza kununua ndege mbili mpya pamoja na kuendelea kuboresha usimamizi wa Shirika.

Mheshimiwa Spika, Reli ya TAZARA ina uwezo mkubwa wa kubeba mizigo, kwa kuwa reli hiyo ina viwango vya ratili 80 lakini bado haijaweza kuleta manufaa kwa kiwango kinachopaswa. Reli hiyo imeshindwa kujiendesha kibiashara kutokana na baadhi ya wadau wa nchi jirani kutoitumia kabisa. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Zambia kuendelea kuelimisha wadau husika kuhusu ubora wa Reli hiyo ili kurejesha imani kwa watumiaji na hivyo kuweza kujiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na mipango mizuri ya Serikali ya kuendelea kujenga barabara za lami katika maeneo mbalimbali nchini, Kamati inaona ni vema Serikali ikaweka mkazo zaidi katika kuboresha miundombinu ya barabara katika maeneo ya kimkakati ili kuchochea maendeleo ya kiuchumi kwenye maeneo husika. Kwa mfano barabara kuelekea katika Mbuga na Hifadhi za wanyama hasa zilizopo mikoa ya kusini mwa nchi yetu, za maeneo yanayozalisha chakula kwa wingi, zile zinazoelekea kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji na kwenye miradi mikubwa ya kimkakati bado hazijatumika ipasavyo katika

kuchangia kukuza uchumi wa nchi yetu. Uimarishaji wa barabara kwenye maeneo haya ya kimkakati yataiwezesha Serikali kupata fedha zaidi na hivyo kuendelea kuboresha miundombinu katika maeneo mengine yaliyobakia.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na nchi yetu kuwa na fursa nzuri za kijiografia, bado hatujaitumia fursa hiyo ipasavyo. Kumekuwepo na hatua nzuri zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha bandari ya Dar es salaam, juhudi hizo hazitoshelezi kuwezesha nchi yetu kuwa “gateway” katika ukanda huu wa Afrika mashariki na Kati kama ilivyo kwa jiji laHongkong kwa upande wa Asia ya Mashariki. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka ukarabati na ujenzi wa gati 13 na 14, uboreshaji wa miundombinu ya usafirishaji katika bandari pamoja na kuboresha mfumo mzima wa kuhudumia wateja ili kutoa fursa kwa nchi jirani kutumia bandari yetu ili kukuza uchumi wa nchi yetu.

4.6. Ugharamiaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Kamati inapata shakani namna gani Serikali imejipanga katika kutekeleza Mipango yake kikamilifu. Takwimu zinaonyesha kwamba katika mipango yote iliyopita kuanzia ule wa 2011/12-2015/16; miradi mingi haijaweza kutekelezwa kwa ukamilifu. Bado kuna tatizo kwa upande wa Serikali katika kupata fedha za kugharamia miradi husika, pia

ushiriki mdogo wa Sekta Binafsi katika utekelezaji wa miradi hiyo ambayo Serikali ilitegemea kupata mchango mkubwa kutoka kwao.

4.7. Maoni ya jumla

Mheshimiwa Spika, Pamoja na maoni na ushauri huu uliojikita katika maeneo mahsusi, Kamati ingependa kutoa maoni ya jumla yafuatayo;

- Serikali iziongezee mtaji Benki ya TIB na TADB ili ziongeze uwezo wake wa kuwakopesha wajasiriamali na wakulima.
- Pamoja na kutambua kuwa Dunia sasa ipo katika mfumo wa soko huria, nchi zote duniani zimekuwa na utaratibu wa kulinda masoko ya bidhaa zake. Serikali iweke mkakati kuhakikisha bidhaa ambazo si za lazima sana au bidhaa ambazo zinaweza kutengenezwa hapa nchini kama vile toothpick, maziwa, nyama, tomato sauce, samaki, unga wa mahindi na ngano, mchele n.k haziingizwi nchini kwa kuweka kodi kubwa ya uingizaji wa bidhaa hizo.

- Serikali ichague maeneo machache ya miradi ya maendeleo ya kipaumbele ambayo itaweza kuyakamilisha kwa kuzingatia uwezo wake wa fedha ili iyakamilishe hayo kwa ukamilifu ndipo indelee na maeneo mengine badala ya kuwa na miradi mingi sana na hivyo kufanya utekelezaji wake kuwa mgumu.
- Serikali ifanye mazungumzo na wamiliki wa viwanda vyote vilivyokufa ili kuona namna bora ya kuvifufua kwa viwanda vinavyoweza kufufuliwa.
- Kamati inaunga mkono mpango wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo kutoa mikopo ya muda mfupi, kati na mrefu katika Sekta ya Kilimo pamoja na kugharamia miundombinu ya umwagiliaji, huduma za maghala na usafirishaji. Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kuwa na mkakati maalum wa kuandaa mashamba makubwa na madogo kwa kuyapima ili kuweza kuwavutia wawekezaji na kuondoa migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikitokea mara kwa mara katika maeneo mengi kwa wananchi kuvamia mashamba yaliyotelekezwa.
- Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na umwagiliaji ishirikiane na Sekta Binafsi kuanzisha minada ya mazao ya biashara kama vile Chai ili kurahisisha upatikanaji wa soko kwa wakulima wetu.

- Serikali iangalie uwezekano wa kuondoa baadhi ya kodi na tozo zilizopo katika sekta ya kilimo. (Mfano kuna tozo zipatazo 37 katika zao la chai pekee.)
- Serikali ilifanyie marekebisho ratiba yake ya uandaaji wa mpango wa maendeleo wa Taifa, 2017/18 ili kuwezesha ufanisi wa kutoa mapendekezo ya mpango kwa mwaka husika.
- Serikali ikamilishe haraka mpango wake wa kurasimisha biashara na mali za wanyonge ili kuziongezea thamani, kuwawezesha waweze kukopa katika taasisi za kifedha lakini pia kuwezesha Serikali kukusanya kodi.
- Kamati imegundua kuwa bado kuna uhitaji mkubwa wa Sare za Askari wetu. Kamati inaona ili kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili Serikali iliwezeshe kifedha Jeshi la Magereza ili liweze kuboresha viwanda vyake vya kuzalisha nguo (Sare) na viatu. Viwanda hivi vizalishe sare za majeshi yote, sare za shule za Serikali za Msingi, sekondari na Vyu vya Ufundi, Sare za Manesi na madaktari pamoja na Sare za wafungwa.

- Kamati inashauri, kwa kuwa NSSF ilishawekeza dola za Kimarekani milioni kumi (10) katika kiwanda cha General Tyre basi wapewe nafasi ya kukiendeleza kiwanda hiki. Serikali iwakutanishe General Tyre, TIB na NSSF ili waone namna bora ya kukifufua kiwanda hiki
- Kamati inashauri NDC iruhusiwe kukopa au kushirikisha na Mifuko ya Hifadhi ya jamii au Benki za ndani kama CRDB, TIB ili kwa pamoja wawekeze katika mradi wa Kuhusu Kiwanda cha magadi Soda.

5.0 HITIMISHO


Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika kwa miongozo yenu ambayo mmekuwa mkitupatia Wabunge. Namshukuru Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Philip Mpango, Mb na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Nawashukuru pia wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili Mapendekezo ya Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka pamoja na mwongozo kwa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe waKamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali yaliyohusu masuala hayo mawili muhimu. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo;

1. Mhe. Hawa A. Ghasia, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Josephat S. Kandege, Mb - M/Kiti
3. Mhe. Hamida Mohamedi Abdallah, Mb
4. Mhe. Jitu V. Soni, Mb
5. Mhe. Jerome Bwanausi, Mb
6. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
7. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
8. Mhe. Maria Ndila Kangonye, Mb
9. Mhe. Susan Peter Maselle, Mb
10. Mhe. Augustino Manyanda Masele, Mb
11. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
12. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb
13. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
14. Mhe. Janet Zebedayo Mbene, Mb
15. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb
16. Mhe. Susana Chogisasi Mgonukulima, Mb
17. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb
18. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
19. Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
20. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
21. Mhe. David Ernest Silinde, Mb

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri pamoja na Sekretariati ya Idara ya Kamati ya Bajeti kwa kuihudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.



Hawa A. Ghasia, Mb

MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI

01 Novemba, 2016